# Sababu za kukwama kwa sekta ya viwanda (2)



Sukari ni moja ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani nchini. **Picha ya Maktaba.**

**HABARI ZAIDI**

**-Sera ya Mpango wa Maendeleo (SIDP) ya mwaka 1996-2020 inazuia kuwapo kwa uzalishaji viwandani hasa kwa wajasiriamali wapya.**

**-Katika Mkoa wa Arusha na Kilimanjaro, viwanda vingi ambavyo vilitaifishwa chini ya SIDP vilikufa.**

**-SIDP ilitoa fursa muhimu kwa wauzaji pembejeo wa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, lakini viwanda vyote vilikufa.**

**-Pamoja na uzoefu uliopatikana kwa kushindwa kwa awamu ya kwanza ya SIDP, serikali iliendelea kutekeleza awamu ya pili bila kufanya utafiti au kuuliza wenye viwanda na umma.**

**Gharama za kuzalisha bidhaa mbalimbali nchini ni kubwa kutokana na kuwapo miundombinu mibovu**

Veneranda Sumila,Mwananchi

SEKTA ya viwanda ina uwezo mkubwa wa kubadilisha uchumi wa Tanzania na kuwa bora na endelevu kama serikali itachukua hatua ya kubadilisha sera, taratibu na kanuni ili kupata mfumo thabiti wa kuinua viwanda.

Wataalamu hao wamesema sekta ya viwanda ndio sekta pekee ambayo haina uratibu wala mwelekeo wa pamoja.

"Sekta imejaliwa kuwa na taasisi mbalimbali zenye wafanyakazi wa kutosha, lakini hazina mwelekeo wa pamoja," anabainisha Mshauri wa Ujasiriamali, Biashara na Menejimenti ya Mazingira, Geoffrey Kalugendo.

Utafiti umezitaja taasisi zenye wafanyakazi wa kutosha ni; Engineering and Manufacturing Design Organization - TEMDO, IPI, Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA)

Kalugendo anasema pamoja na taasisi hizo kuwapo kwa muda mrefu, hazina mkakati wa pamoja wa kuwawezesha wajasiriamali wa chini na wa kati kutumia mkakati wa pamoja.

**TFDA ina maabara moja tu**

Utafiti uliofanywa na Shirikisho la Wafanyabiashara, Kilimo na Wenye Viwanda Tawi la Arusha (TCCIA-Arusha) uliojikita kwenye masuala ya kiufundi, unabainisha kwamba licha ya Wakala wa Chakula na Dawa nchini (TFDA) kusimamia masuala ya afya nchini, ina maabara moja tu ambayo ipo makao makuu ya wakala jijini Dar es salaam.

Utafiti huo unaonyesha kwamba maabara moja haitoshi huku ofisi ya Arusha ikiwa imezidiwa na kazi kutokana na kuwa na wafanyakazi wachache.

Kwa mujibu wa utafiti huo Shirika la Viwango nchini (TBS) halina ofisi mkoani Arusha wala Moshi na kwamba wanapoangalia viwango ubora wa bidhaa mbalimbali, maofisa wanalizimika kutoka jijini Dar es Salaam.

Kutokana na upungufu huo wazalishaji wa Tanzania wako huru kuzalisha bidhaa kwa viwango vyao ambavyo vinashindwa kuingia katika Soko la Afrika Mashariki.

Akizungumza na Mwananchi kwa njia ya simu, Kalugendo anasema suala linalokwamisha maendeleo yao ni kukosekana kwa utaalamu wa ujasiriamali kutoka kwa baadhi ya wataalamu wa serikali.

Anasema kwamba sekta ya viwanda inapata shida kubwa kutokana na maofisa kujifanya mabosi na kushindwa kujichanganya na wafanyabiashara na wakulima.

Kalugendo amewashauri maofisa wa serikali kuwatia elimu ya ujasiriamali ili kusukuma mbele uchumi wa Tanzania.

Anasema tabia ya wafanyakazi wa serikali kukaa maofisini, hawafanikiwa kuleta mabadiliko katika uchumi wa Tanzania.

"Serikali na maofisa wake ni lazima wabadili fikira zao katika sekta binafsi kutokana na ukweli kwamba inatengeneza ajira hasa kwa vijana ambao wengi hawana kazi," anasema Kalugendo. Utafiti huo pia umetaka utaalamu wa maofisa waliopo kwenye taasisi zinazosaidia sekta ya viwanda waboreshe utaalamu wao.

Pia utafiti umetaka TCCIA kupanua zaidi huduma zake kwa kushirikisha sekta ya viwanda, kilimo na biashara, wanasiasa ili kuleta maendeleo kwenye sekta ya viwanda.

Kalugendo anasema washirika muhimu kwa mfano, sekta ya viwanda kama TCCIA, VETA, TIRDO, Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) na SIDO wanapaswa kutoa mafunzo na kuwashawishi wajasirimali wapya kutambua fursa zilizopo katika Soko la Pamoja la Afrika Mashariki (EACM).

Fursa hizo ni pamoja na kuunganisha nguvu zao na kuzitumia kununua rasilimali kama kiwanda cha Kiltex na Ghala la Usagishaji la Taifa.

Utafiti huo pia umehimiza TCCIA kwa kushirikiana na TBS na mamlaka nyingine za sheria na kanuni, kutoa mafunzo kwa umma kuhusu sera zilizopo kwenye viwanda, sheria na viwango katika sekta ya viwanda.

Kwa miaka mingi sekta ya viwanda imekabiliwa na changamoto nyingi. Moja ya changamoto hizo, ni tatizo la umeme. Viwanda vya Tanzania vimeathirika kwa kukosa nishati ya kudumu ya umeme na kupanda kwa bei za mafuta ya petroli na gesi.

Tatizo la umeme limewavuruga zaidi wajasirimali wapya katika sekta ya viwanda.

Kutokana na tatizo la umeme, zaidi ya nusu ya taasisi zinamiliki majenereta ambayo wanayategemea kwa asilimia 10 kuendesha shughuli zao. Nishati ya jenereta ni ghali mara tatu kuliko nishati ya umeme wa kawaida.

**Barabara**

Miundombinu ni jambo muhimu katika kuamua aina ya uzalishaji unaotakiwa kufanyika viwandani na bei ya mwisho ya mauzo; lakini kutokana na kutegemea zaidi barabara kumesababisha uzalishaji kuwa gharama kubwa.

Uzalishaji unakuwa gharama kubwa kutokana na kuwapo kwa miundombinu mibovu ya barabara hasa katika kipindi cha mvua, hazipitiki.

Mbali na kuwapo kwa matatizo hayo kuna matumaini ya kuwapo kwa gharama nafuu za kutokana na serikali kutangaza kujenga reli ya kati.

Tabia ya sasa ya kutumia malori inaleta hasara kubwa kutokana na bei ya mafuta , spea, kuharibika kwa barabara na gharama zote kubeba mlaji.

**Tujadiliane kupitia Ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni Bure, hautozwi!**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI